# MAJARIBIO YA MTIHANI DARASA LA SABA

# MUHULA WA KWANZA-KISWAHILI-2019

*1. Hakikisha umeandika* **MUDA: SAA 1 DAK. 40**

***(i)Jina lako*** ***(ii)Jina la shule yako***

---

**Soma vifungu vifuatavyo. Kwa kila nafasi, umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo zaidi .**

Kenya ni taifa __1__ makabila mengi sana. Kiswahili __2__ lugha __3__ Wakenya __4__ wa matabaka __5__ __6__ kujali umri au jinsia. Bila __7__ bila Kiswahili Kenya __8__ kama mnara wa Babeli. Kiswahili ni lugha ya __9__ __10__ imeleta utangamano miongoni mwa Wakenya wenye asili tofauti.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. penye | B. yenye | C. kwenye | D. lenye |
| **2.** | A. ndio | B. ndiyo | C. ndizo | D. ndicho |
| **3.** | A. zinazowaunganisha | B. inaowaunganisha | C. inayowaunganisha | D. inayounganisha |
| **4.** | A. wowote | B. wote | C. wote wote | D. kote |
| **5.** | A. mbalimbali | B. bali bali | C. mbali mbali | D. balibali |
| **6.** | A. wala | B. ila | C. bila | D. ama |
| **7.** | A. shaka | B. saka | C. zaka | D. ukweli |
| **8.** | A. itakuwa | B. kungukuwa | C. kutakuwa | D. ingekuwa |
| **9.** | A. mataifa | B. taifa | C. kitaifa | D. ulimwengu |
| **10.** | A. ambazo | B. ambalo | C. ambayo | D. ambao |

__11__ ya hayo, tukumbuke __12__ hakuna kizuri kisichokuwa na __13__. Kuna __14__ ya mila zinazopaswa kupigwa teke __15__ kuwarithi wake kwa shuruti au kuwakeketa wasichana.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| **11.** | A. Kati | B. Licha | C. Baina | D. Pamoja |
| **12.** | A. kua | B. kuwa | C. vile | D. kwa |
| **13.** | A. mwenyewe | B. ukamili | C. sawa | D. dosari |
| **14.** | A. ndani | B. kati kati | C. baadhi | D. juu |
| **15.** | A. mathalani | B. maadam | C. fauka ya | D. sembuse |

**Kutoka swali la 16 hadi 30, jibu swali ukifuata maagizo uliyopewa.**

**16. Ni sentensi ipi yenye maana tofauti na nomino yenyewe?**

A. Topasi - Husafisha misala
B. Nyakanga - Kiongozi wa makungwi
C. Ngariba - Anayepasha tohara
D. Mshenga - Apelekaye barua benki

**17. Tambua kielezi idadi katika sentensi ifuatayo:-**

Wanafunzi watano walikubali kabisa kurudi kuchota maji mara tano kabla ya giza kuingia.

A. walikubali kabisa  B. kabla ya
C. mara tano  D. Wanafunzi watano

**18.** Chagua kiumbe aliyeambatanishwa sawa sawa na makao yake.

A. Kiwavi - Nyasini
B. Nyuki - Masega
C. Panzi - Koa
D. Mtawala - Kitala

**19.** Ni kimelea yupi anayefanana na nyungunyungu, hufyonza damu na hukaa maeneo ya majimaji?

A. Ruba  B. Ndorobo
C. Chafuo  D. Pange

**20.** ________ hupelekwa rumande kufuatana na amri ya hakimu.

A. Mahabusu  B. Mtuhumiwa
C. Mfungwa  D. Mdhamini

Compiled and distributed online by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Nairobi. Tel:+254202319748 |
E-mail: infosnkenya@gmail.com | Order answers online at www.schoolsnetkenya.com

21. Chagua methali yenye uhusiano na ifuatayo.
A. Polepole ndio mwendo
B. Aliyekupatia kiti ndiye aliyenipa kumbi
C. Haraka haraka haina baraka
D. Pwagu humpata pwaguzi

22. Kumshika mtu miguu ni sawa na ________.
A. kumbeza mtu B. kumrudisha nyuma
C. kumheshimu mtu D. kukata mtu mwendo

23. Maji yalimwagika mwaa kukawa kunateleza parr. Sentensi hii imetumia fani gani ya lugha?
A. Tashbihi B. Tanakali
C. Tathlitha D. Utenzi

24. Shaba, almasi, dhahabu, misitu na chemichemi kwa pamoja ni __________.
A. madini B. mali asili
C. maumbile D. mali ghusi

25. Maumivu ya mifupa au viungo kwa sababu ya baridi shadidi ni ___________.
A. kinarusi B. ukoma
C. kichocho D. baridi yabisi

26. **Chagua kauli ya kutendesha ya sentensi ifuatayo.**
Nilinawa mikono kwa maji baridi.
A. Nilinawisha mikono kwa maji baridi.
B. Niliunawia mikono kwa maji baridi
C. Nilinawika mikono kwa maji baridi.
D. Nilinavya mikono kwa maji baridi.

27. Mtu anayewatumikisha wengine ilhali yeye amestarehe tu ni
A. Kabwela B. Kabaila
C. Kabili D. Kaburu

28. **Chagua wingi wa sentensi:-**
Uzi huo umeutoa wapi?
A. Nyuzi hiyo umeitoa wapi?
B. Uzi hizi umezitoa wapi?
C. Nyuzi hizo mmezitoa wapi?
D. Uzi hizo mmitoa wapi?

29. Chagua jibu linaloonyesha mfululizo unaofaa wa nyakati za usiku.
A. Adhuhuri, machweo, macheo, alasiri
B. Macheo, adhuhuri, alasiri, macheo
C. alasiri, adhuhuri, macheo, machweo
D. macheo, adhuhuri, alasiri, machweo

30. **Kanusha wa sentensi:-**
Angalikwenda kwake asubuhi angalimkuta.
A. Asingalikwenda kwake asubuhi asingemkuta.
B. Hangekwenda kwake asubuhi hangemkuta.
C. Asingalikwenda kwake asubuhi asingalimkuta.
D. Asingekwenda kwake asubuhi asingemkuta.

**<u>Soma ufahamu ufuatao kwa makini kisha ujibu maswali 31 - 40.</u>**

Umati mkubwa ulikuwa umesongamana katika uwanja mpana wa boma la mfalme Msa. Walioalikwa wote walihudhuria. Baada ya hotuba mbalimbali kutolewa wakati iliwadia wa kuonyesha ukarimu wa vidole na meno na matumbo. Kila mtu alianza kumeza mate. Hata hivyo, iliwabidi wasubiri kidogo, kwani subira huvuta heri. Wapishi na waandalizi walianza kuandaandaa vyombo mezani katika uwanja.

Sufuria kubwa za maakuli pale, sinia la wali pale, mabakuli ya michuzi rojorojo pale, majagi ya maji safi na mabuzi ya kahawa na chai huku na kule.

Mfalme Msa, msemaji maarufu wa karne yake alisimama kwa maungo kama tausi akasema, "Ndugu wapenzi, ningependa kuchukua fursa hii kuwafafanulia maana ya neno maisha. Neno maisha latokana na muungano wa maneno mawili. Yaani mambo na isha. Kwa hivyo maneno haya mawili tunapata siri ya maisha kuwa ni mambo yanayoisha. Tumekutana tule tushibe sana. "Ulacho ndio chako."

Amri ikatolewa chakula cha wageni kiletwe. "Nyama nzuri kuliko zote kwanza." Mpishi akaandaa nyama kwa adabu kubwa, "Hii hapa nyama nzuri kuliko zote." Sulemani akasema kwa kweli ilikuwa nyama nzuri zaidi ya hivyo, ilipikwa kwa ujuzi wa hali ya juu kupita kiasi. Walaji waliramba vidole ovyo. Watu walishangaa. Wengi wengine walitaka kujua zilikuwa ndimi za wanyama gani. Labda wawe ni wanyama wasio wa kawaida. Wageni ndio waliofurahia kuliko wote. Kwani sherehe ilikuwa ni kwa ajili yao.

Bandubandu huishia gogo. Mara nyama tamu ikaisha. "Sasa leta nyama mbaya," mfalme aliamuru. Sulemani na kikosi chake hawakukawia. Nyama mbaya ikaandaliwa mezani. Na kweli ilikuwa mbaya vipande vya nyama vilivyokatwa ovyo ovyo tu. Viungo navyo si lolote si chochote. Supu ni kama maji ya kidimbwi.

Nyama hiyo haikuwa na ladha hata kidogo. Kila mtu aliamini kuwa duniani kuna nyama mbaya, udadisi ukaanza. "Nyama gani hii?"

Misingi madhubuti ya kinidhamu hujengwa tangu watoto wakianza kutambua mambo. Kungoja mpaka mtoto awe mkubwa ndio aanze kufunzwa maadili ni kama kujaribu kumkunja samaki akiwa tayari amekomaa na kuwa mkavu; **udongo tuuwahi uli maji.**

Hapo kale mambo yalikuwa tofauti, mtoto aliweza kukosolewa na mtu yeyote yule hata kama alikuwa ni mpita njia. Watoto walikuwa ni wa jamii, hulka zao zilionekana mapema kama vile nyota njema zionekanavyo alfajiri. Watoto walikuwa wakitenda mambo huku wakijihisi kuwa wanakodolewa macho na jamii. Hisia hizo ziliwafanya watoto kujichunguza, kujiasa na kutenda kila jambo kwa tahadhari. Watoto waliwaheshimu watu wazimu bila kushurutishwa, hali ambayo ilijenga uhusiano mzuri katika jamii.

Mtoto afunzwaye adabu ipasavyo kawaida hawezi kuterereka popote alipo, iwe shuleni au nyumbani. Mtoto kama huyo kufanya zumbukuku na watovu wa nidhamu sio rahisi, bali ataweza kuchukua nafsi ya walimu na wazazi kuyapitisha maadili mwafaka kwa wenzake. Mtoto huyo hukuza mbegu bora katika jamii. Yeye hujistahi, huwa na bidii na uvumilivu mwingi.

Tuache ubaguzi, uvivu na ubinafsi ili kuwapa watoto mifano bora na miangaza ya kuwakuza kifikira, kielimu, kiuchumi na kitamaduni. Jamii isipuuze kutoa michango yake katika urekebishaji wa watoto. **Mathalani**, ni makosa mtu kuacha kumkosoa mtoto atendaye mambo ya kuhatarisha maisha yake na ya wenzake.

Watoto hata nao wana jukumu katika kuyaimarisha maisha yao. Wanapaswa kuziepuka tabia zote mbaya hata ikiwa hawapewi misingi makwao. Wanaweza kuziiga jamii nyoofu kinidhamu hata ikiwa sio wazazi wao na kuyatupilia mbali mambo maovu ambayo yanawazunguka katika jamii. Ni vizuri wajue kuwa urithi bora ni ule wa kuiga tabia nzuri, bidii na kupata elimu yenye manufaa.

**41.** Kulingana na aya ya kwanza __________.
A. jamii imara huhitaji misingi madhubuti
B. jamii thabiti haihitaji misingi madhubuti
C. wazazi hawaisimamishi misingi ya malezi
D. wazazi wasiwatambue warithi

**42.** Neno ***"warithi!"*** limetumika katika ufahamu. Maana yake ni __________.
A. wanaoridhika na mali
B. wanaomiliki mali ya mtu aliyestafu
C. wanaomiliki mali ya mtu aliyekufa
D. wanaohusiana na mtu aliye na mali

**43.** Vijana wanapaswa kuelewa umuhimu gani katika aya ya pili?
A. Kurithi mali
B. Kulijenga jumba la ghorofa
C. Kuupokea uongozi
D. Msingi wa nidhamu

**44.** Misingi ya kinidhamu hujengwa lini?
A. Mpaka mtoto awe mkubwa zaidi
B. Mtoto akiacha kutambua mambo
C. Tangu watoto wakianza kufumba mambo
D. Toka mtoto akianza kutambua mambo

**45.** Maana ya **"udongo tuuwahi uli maji"** ni____.
A. kukomaa na kuwa mkavu
B. tuchanganye udongo na maji
C. tutende jambo mapema kabla halijaharibika
D. kumkunja samaki

**46.** Watoto wa zamani ___________.
A. walilelewa kwa ugumu
B. walilelewa kwa ushirikiano
C. waliheshimiwa na watu wazima
D. walikosolewa na mzazi tu

**47.** Mtoto afunzwaye adabu ipasavyo _______.
A. hawezi kushawishika
B. hawezi kubabaika
C. hawezi kutetemeka
D. hawezi kupotoka

**48.** Chagua jibu lenye maana sawa na **"mathalani"** kama lilivyotumiwa katika kifungu.
A. Kwa mfano B. Kwa kweli
C. Kwa sababu D. Kwa kuwa

**49.** Mtoto anapokuza mbegu bora katika jamii hufanya haya yote ila ___________.
A. yeye hajiamini
B. yeye huwa na bidii
C. yeye hujiheshimu
D. yeye huwa na uvumilivu

**50.** Kwa mujibu wa kifungu, chagua jibu sahihi.
A. Watoto walishurutishwa kuheshimu watu wazima
B. Watoto walitenda kila jambo kwa tahadhari
C. Watoto wasiweze kuziiga jamii nyoofu kinidhamu
D. Watoto hawakukosolewa na mtu yeyote